# Zana ya Kutathmini Umaskini
# ya Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini
# Burundi
## Simple Poverty Scorecard® Poverty-Assessment Tool

Mark Schreiner

31 Oktoba 2017

Ce document en Français est disponible sur `SimplePovertyScorecard.com`
Iyi nyandiko iboneka mu Kirundi kuri `SimplePovertyScorecard.com`
This document in English is available at `SimplePovertyScorecard.com`.
Hati hii na zana husika zimo kwa lugha ya Kiswahili kwenye `SimplePovertyScorecard.com`

## Muhtasari

Zana ya kutathmini umaskini nchini Burundi ya Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini (*Simple Poverty Scorecard® poverty-assessment tool*) inatumia viashiria 10 vya gharama za chini kutoka kwenye utafiti wa Ênquête sur les Conditions de Vie des Ménages wa mwaka wa 2013/14 ili kukadiria uwezekano kwamba kaya ina matumizi ya chini ya mstari fulani wa umaskini. Wafanyakazi wa uwandani wanaweza kukusanya majibu kwa takriban dakika kumi. Usahihi umeripotiwa kwa mistari mbali mbali ya umaskini. Kadi ya alama ni njia fanisi kwa mipango ya kuwasaidia maskini nchini Burundi ya kukadiria viwango vya umaskini, ili kufuatilia mabadiliko katika viwango vya umaskini baada ya muda, na ili kuainisha wateja kwa ajili ya huduma zilizobinafsishwa.

## Shukrani

Data zimetolewa kwenye *Institut de Statistiques et des Études Économiques du Burundi*. Shukrani kwa Nadia Belhaj Hassine Belghith, Nicolas Ndayishimiye, Noé Nduwabike, Mélance Nibigira, Jeanine Niyukuri, na Jean Paul Sossou. Tafsiri ya Kiingereza hadi Kiswahili imefanywa na George Karanja (`mail@georgekaranja.com`). “Simple Poverty Scorecard” is a Registered Trademark of Microfinance Risk Management, L.L.C. Copyright © 2017 Microfinance Risk Management.

## Mwandishi

Mark Schreiner ni mkurugenzi wa Microfinance Risk Management, L.L.C. Pia yeye ni Senior Scholar katika Center for Social Development katika Washington University in Saint Louis.

# Zana ya Kutathmini Umaskini ya Kadi Rahisi ya Alama za Umaskini

| | | | Jina | Kitambulishi |
|---|---|---|---|---|
| Na. ya mahojiano: | | | | |
| Tarehe ya mahojiano: | | Mshiriki: | | |
| Nchi: | BDI | Ajenti wa wandani: | | |
| Kadi ya alama: | 001 | Kituo cha huduma: | | |
| Sampuli ya uzani: | | Idadi ya jamaa wa kaya: | | |

| Kiashiria | Jibu | Alama | Score |
|---|---|---|---|
| 1. Ni jamaa wangapi wa kaya wana umri wa miaka 18 au chini? | A. Sita au zaidi | 0 | |
| | B. Wanne, au watano | 3 | |
| | C. Watatu | 6 | |
| | D. Wawili | 9 | |
| | E. Mmoja | 13 | |
| | F. Sifuri | 19 | |
| 2. Jamaa wote wa kaya wenye umri wa miaka 7 hadi 16 wanaenda shule au kituo cha elimu hivi sasa (katika mwaka huu wa shule)? | A. La | 0 | |
| | B. Ndiyo | 3 | |
| | C. Hakuna jamaa wenye umri wa miaka 7 hadi 16 | 6 | |
| 3. Miongoni mwa jamaa wa kaya wenye umri wa miaka 10 au zaidi waliofanya kazi kwa angalau saa 1 katika siku 7 zilizopita, je, ni wangapi kazi yao kuu (au kazi yao ya kawaida) ilikuwa katika sekta ya kilimo, ufugaji wanyama, au uvuvi? | A. Watatu au zaidi | 0 | |
| | B. Wawili | 5 | |
| | C. Mmoja, au hakuna | 9 | |
| 4. Ikiwa kiongozi/mwanandoa wa kiume alifanya kazi kwa angalau saa 1 katika siku 7 zilizopita, basi kazi yake kuu (au kazi yake ya kawaida) ilikuwa katika sekta ya kilimo, ufugaji wanyama, au uvuvi? | A. Hakufanya kazi | 0 | |
| | B. Alifanya kazi katika kilimo n.k. | 4 | |
| | C. Hakuna mwanandoa/kiongozi wa kiume | 7 | |
| | D. Alifanya kazi isiyohusiana na kilimo | 11 | |
| 5. Kiongozi/mwanandoa wa kike anaweza kusoma na kuandika maandishi rahisi kwa lugha ya Kirundi, Kifaransa, Kiswahili, au lugha nyingine? | A. Hakuna kiogozi/mwanandoa wa kike | 0 | |
| | B. La | 1 | |
| | C. Kirundi pekee | 2 | |
| | D. Kifaransa, lakini si Kiswahili, au lugha nyingine (bila kuzingatia Kirundi) | 4 | |
| | E. Kiswahili, au lugha nyingine (bila kuzingatia Kirundi na Kifaransa?) | 7 | |
| 6. Kaya inatumia choo cha aina gani? | A. Mtaro wazi, choo cha shimo cha umma, choo cha jirani, au aina nyingine | 0 | |
| | B. Choo cha shimo chenye hali mbaya | 4 | |
| | C. Choo cha kumwagwa maji (ukitumia bomba au mikono) au choo cha shimo chenye hali nzuri | 12 | |
| 7. Kaya inatumia aina gani ya moto kwa mapishi? | A. Kuni za kuokotwa, au samadi | 0 | |
| | B. Kuni za kununuliwa, au nyingine | 1 | |
| | C. Makaa, gesi, stima, mafuta taa, au hawapiki | 11 | |
| 8. Kaya inatumia chanzo gani kuu cha mwangaza? | A. Kuwasha kuni, au nyingine | 0 | |
| | B. Taa ya kutengenezewa nyumbani inayotumia mafuta taa na haina glasi (*koroboi*), au gesi | 5 | |
| | C. Taa ya mafuta taa yenye glasi, miale ya jua, au mishumaa | 9 | |
| | D. Stima, au jenereta | 15 | |
| 9. Kaya yako ina simu ya rununu kwa sasa? | A. La | 0 | |
| | B. Ndiyo | 7 | |
| 10. Kaya yako ina redio kwa sasa? | A. La | 0 | |
| | B. Ndiyo | 3 | |

 **Score:**

# Lahakazi ya Ukurasa wa Nyuma: Jamaa wa Kaya, Umri, Kuenda Shule, Hali ya Kikazi, na Kazi katika Kilimo

Jaza kichwa cha kadi ya alama kwanza. Jumuisha kitambulishi cha kipekee cha mahojiano (ikiwa kinajulikana), tarehe ya mahojiano, na sampuli ya uzani wa mshiriki (ikiwa unajulikana). Kisha urekodi jina kamili na nambari tambulishi ya kipekee ya mshiriki (ambaye anaweza kuwa mtu tofauti na mhojiwa), ya ajenti wa uwandani wa mshiriki (ambaye anaweza kuwa mtu tofauti nawe mhoji), na ya kituo cha huduma kinachotumiwa na mshiriki.

Kisha umsomee mhojiwa: *Tafadhali nieleze majina ya kwanza (au lakabu) na umri wa jamaa wote wa kaya yako, ukianzia na kipngozi na mwanandoa wake (mwenye umri wa juu zaidi).* Kaya *ni kundi la watu au mtu mmoja—bila kujali uhusiano wa damu au ndoa—ambao kwa kawaida wanashiriki milo, wako chini ya uongozi wa jamaa mmoja wa kaya (anayejulikana kama* kiongozi wa kaya*), na anayeshiriki mapato na gharama. Kundi hili la watu kwa kawaida wanaishi katika nyumba moja na chini ya paa moja.*

Andika jina/lakabu na umri wa kila jamaa, na uonyeshe kiongozi, jinsia yake, na mwanandoa (mwenye umri wa juu zaidi) wa kiongozi (ikiwa yupo). Unahitajika kujua umri hasa wa jamaa ikiwa tu umekaribia miaka 7, 10, au 16. Rekodi idadi ya jamaa wa kaya kwenye kichwa cha kadi ya alama karibu na eneo lililoandikwa “Idadi ya jamaa wa kaya:”, na kisha uweke mduara kwenye jibu la kiashiria cha kwanza cha kadi ya alama.

Kwa kila jamaa mwenye umri wa miaka 7 hadi 16, uliza kama wanaenda shule au kituo cha elimu hivi sasa (katika mwaka huu wa shule). Kisha uweke mduara kwenye jibu la kiashiria cha pili. Weka alama kwenye “C. Hakuna jamaa wenye umri wa miaka 7 hadi 16” ikiwa hakuna jamaa wenye umri wa miaka 7 hadi 16. Weka alama kwenye “B. Ndiyo” ikiwa kuna jamaa wenye umri wa miaka 7 hadi 16 na ikiwa wote wanaenda shule. Weka alama kwenye “A. La” ikiwa kuna jamaa wenye umri wa miaka 7 hadi 16 na angalau mmoja wao haendi shule.

Kwa kila jamaa ambaye ana umri wa angalau miaka 10, uliza kama alifanya kazi kwa angalau saa 1 katika siku 7 zilizopita, na urekodi jibu. Kwa kila jamaa ambaye alifanya kazi, basi uliza kama kazi yake kuu (au kazi yake ya kawaida) ilikuwa katika sekta ya kilimo, ufugaji wanyama, au uvuvi, na urekodi jibu. Kisha uweke mduara kwenye viashiria vya tatu na nne vya kadi ya alama.

Kila wakati kumbuka na utumie maagizo ya kina yaliyo kwenye “Miongozo ya Mahojiano”.

| Jina la kwanza (au lakabu) | [JINA] ndiye kiongozi au mwanandoa (mwenye umri wa juu zaidi) wa kiongozi? | [JINA] ana umri gani? | Ikiwa [JINA] ana umri wa miaka 7 hadi 16, je, anaenda shule au kituo cha elimu hivi sasa (katika mwaka huu wa shule)? | Ikiwa [JINA] ana umri wa angalau miaka 10, basi alifanya kazi kwa angalau saa 1 katika siku 7 zilizopita? | Ikiwa [JINA] alifanya kazi, basi kazi yake kuu (au kazi yake ya kawaida) ilikuwa katika sekta ya kilimo, ufugaji wanyama, au uvuvi? |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kiongozi wa kiume<br>Kiongozi wa kike | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 2. | Mwanandoa (mwenye umri wa juu zaidi)<br>Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 3. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 4. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 5. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 6. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 7. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 8. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 9. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 10. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 11. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 12. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| 13. | Nyingine | | <7 au >16 La Ndiyo | <10 La Ndiyo | <10 Hakufanya kazi La Ndiyo |
| Idadi ya jamaa wa kaya: | | — | — | — | Idadi ya wanaofanya kazi katika kilimo: |